

# **Kuorodhesha Haki za Kidijitali nchini Angola, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Jamhuri ya Afrika ya Kati**

**Uchambuzi wa Unitel-Angola, Orange-DRC na Orange CAR**





December 2021

**Waandishi:**

Bulanda T Nkhowani, Rigobert Kenmogne

**Timu ya Wahariri:**

Thobekile Matimbe, Nnenna Paul-Ugochukwu

**Ubunifu na Mpangilio:**

Kenneth Oyeniya

**Mfasiri wa Kiswahili:**

Bonface Witaba



Creative Commons  
Attribution 4.0 International (CC BY 4.0)

# 01



## Utangulizi

Ranking Digital Rights (RDR) hufanya kazi kukuza uhuru wa kujieleza na faragha kwenye Mtandao kwa kuunda viwango vya kimataifa na motisha kwa makampuni kuheshimu na kulinda haki za watumiaji (haki za binadamu)<sup>1</sup>.

RDR inafanikisha hili kwa kuorodhesha majukwaa ya kidijitali yenye nguvu zaidi duniani na makampuni ya mawasiliano kuhusu ahadi na sera husika, kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya haki za binadamu. Timu ya RDR inafanya kazi na makampuni pamoja na watetezi, watafiti, wawekezaji na watunga sera ili kuanzisha na kuendeleza viwango vya kimataifa ya uwajibikaji wa shirika<sup>2</sup>.


Paradigm Initiative inafanya kazi ili kutoa fursa za kidijitali kwa vijana wa Kiafrika na kukuza haki za kidijitali na haki za binadamu zinazo heshimu sheria na sera kote Afrika.

Ni kutokana na hali hii ambapo Paradigm Initiative kushirikiana na Ranking Digital Rights ili kuorodhesha makampuni ya mawasiliano ya simu kufuata viwango vya haki za binadamu katika nchi tatu; Angola, Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR) na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) chini ya Mradi Mkuu wa Uhuru wa Mtandao.

1 Ranking Digital Rights, 2021, <https://rankingdigitalrights.org/about/> (accessed 10th August 2021).

2 Ranking Digital Rights, 2021, <https://rankingdigitalrights.org/about/> (accessed 10th August 2021).

# 02



## Muktadha wa Nchi

### Angola

Angola ni nchi ya Kusini mwa Afrika yenye wakazi milioni 33<sup>3</sup> (2020). Angola ina kampuni tatu za simu za mkononi, Movitel, Unitel na Angola Telecom inayomilikiwa na serikali. Mnamo 2019, ilitangazwa kuwa nchi itakuwa na opereta mpya iitwayo Africell, ambayo inatarajiwa kuzinduliwa mnamo 2022<sup>4</sup>. Kulingana na HootSuite, mnamo 2021 watumiaji wa mtandao walifikia milioni 10, ambayo ni kupenya kwa 31% ya watu wote. Ufikiaji wa simu za rununu una watumiaji zaidi ya milioni 15, ikiwakilisha 46% ya jumla ya watu<sup>56</sup>.

Katika ripoti ya Uhuru kwenye Mtandao ya 2020, Freedom House ilikadiria hali ya uhuru wa mtandao wa Angola kuwa huru kwa kiwango<sup>7</sup>. Hakuna vikwazo vya wazi vya serikali juu ya ufikiaji wa Mtandao na ujumbe wa maandishi. Hakuna visa vinavyojulikana vya serikali kuzuia au kuchuja maudhui ya Mtandao na hakuna vikwazo vinavyojulikana kuhusu aina ya habari au maudhui ambayo yanaweza kubadilishana

3 World Bank, 2020, Angola Country Data, <https://data.worldbank.org/indicator/SP.POP.TOTL?locations=AO> (accessed 10th August 2021).

4 Africell, 2021, <https://www.africell.com/en/markets/angola> (accessed 10th August 2021).

5 Hootsuite, 2021, Digital 2021 in Angola, <https://datareportal.com/digital-in-angola>, (accessed on 20th May 2021).

6 It is important to note that the regulator INACOM does not provide up-to-date data on the use of information and communication technologies in Angola.

7 Freedom House, 2020, Freedom on the Net Report: Angola, <https://freedomhouse.org/country/angola/freedom-net/2020>, (accessed on 20 December 2021).

wakati wa mawasiliano.

Katiba ya Angola<sup>8</sup> inatoa uhuru wa kujieleza na vyombo vya habari, na mnamo Januari 2017 seti ya sheria mpya za vyombo vya habari zinazo julikana kama Kifurushi cha Sheria ya Mawasiliano ya Kijamii, ambacho kinajumuisha Sheria mpya ya Vyombo vya Habari, Sheria ya Televisheni, Sheria ya Utangazaji, Kanuni za Maadili ya Wanahabari, na sheria za kuanzisha. Bodi ya Udhubiti ya Angola ya Mawasiliano ya Kijamii (Entidade Reguladora da Comunicação Social Angolana-ERCA) ilipitishwa. Sheria ya Huduma za Kampuni ya Mawasiliano na Habari ya Kielektroniki inasimamia sekta ya TEHAMA na mawasiliano ya simu na inatoa haki za raia za faragha na usalama mtandaoni.

### **Jamhuri ya Afrika ya Kati**

Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR) ni nchi iliyo katika ukanda wa Jumuiya ya Kiuchumi na Fedha ya Afrika ya Kati (CEMAC) iliyoko Afrika ya Kati. Mnamo 2021, CAR ilikuwa na idadi ya watu takriban milioni 4.9<sup>9</sup>. TNchi imekuwa ikijishughulisha na maendeleo ya miundombinu ya TEHAMA tangu 2020. Waendeshaji wanne wanashiriki soko la wateja wa simu za rununu, ambazo ni Orange, Telecel, Moov na Azur. Kiwango cha kupenya kwa Mtandao ni zaidi ya 43.9% kulingana na Mamlaka ya Udhubiti wa Mawasiliano na Posta (ARCEP)<sup>10</sup>. Waendeshaji hutoa huduma ya simu ya 2G na 3G yenye huduma zinazopatikana miji mikubwa zaidi nchini.

Wakala wa Udhubiti wa Mawasiliano katika Jamhuri ya Afrika ya Kati (ART) ni taasisi iliyopewa uhuru wa kibinafsi wa kisheria na usimamizi kwa mujibu wa Sheria ya 07-020 ya Desemba 28,2007. ART

imekuwa ikifuatilia tangu mwaka 2004, kuhakikisha uangalizi wa kiteknolojia juu ya matumizi ya kanuni na maendeleo na uendelezaji wa sekta ya mawasiliano pamoja na teknolojia ya habari na mawasiliano nchini.

### **Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo**

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) ni nchi ya Afrika ya Kati yenye wakazi wapatao milioni 79. Nchini DRC, soko la simu za rununu linashikiriwa kati ya waendeshaji wa nne: Vodacom, Orange, Airtel Congo na Africell. Katika robo ya pili ya 2021, waendeshaji wanne walifikia milioni 44.85 na kiwango cha ongezeko cha 7.84%<sup>11</sup>. Katika kipindi hicho, kampuni hizi zilirekodi uboreshaji wa kiwango cha kupenya cha karibu 3.7%, ambayo ni, kiwango cha kupenya kiliongezeka kutoka 47.1% hadi 50.8%<sup>12</sup>.

Wahudumu wa simu wanafanya kazi chini ya Sheria mpya n° 20/017 ya tarehe 25 Novemba 2020 inayo husiana na teknolojia ya mawasiliano na habari na mawasiliano ya tarehe 25 Novemba 2020 nchini DRC chini ya uratibu wa Mamlaka ya Posta na Mawasiliano ya Kongo (ARPTC). Ahadi za kampuni kuhusu uhuru wa kujieleza zimeandaliwa na sheria n° 013-2002 ya tarehe 16 Oktoba 2002.

8 Constitution of Angola, Article 40


9 Country Meters, 2021, Central African Republic, [https://countrymeters.info/fr/Central\\_African\\_Republic](https://countrymeters.info/fr/Central_African_Republic), (accessed 24 December 2021).

10 Tableau de bord marchés de télécom, 2020, [https://www.arcep.cf/images/documents\\_divers/observatoires/2020/TAB\\_LEAU\\_DE\\_BORD\\_MARCHES\\_TELECOM\\_RCA\\_Q1\\_2020.pdf](https://www.arcep.cf/images/documents_divers/observatoires/2020/TAB_LEAU_DE_BORD_MARCHES_TELECOM_RCA_Q1_2020.pdf), page 17, (accessed 24 December 2021).

11 Deskeco, millions d'abonnés recensés au 2e trimestre 2021, <https://deskeco.com/2021/11/22/rdc-4485-millions-da-bonnes-actifs-recenses-la-fin-du-2e-trimestre-2021-sur-le-marche-de-la>, (accessed 24 December 2021).

12 Ibid

# 03



## Mbinu

Tathmini ya kampuni za mawasiliano ilifanywa kwa kutumia mbinu ya 2020 RDR ripoti ya uwajibikaji wa kampuni., kwa kuchagua sehemu ndogo ya viashirio kutoka kwa faragha na uhuru wa kujieleza na vipengele vya habari.

Hasa, utafiti huu ulilenga watoa huduma za mtandao wa simu ambao hutoa huduma za data na sauti, na kutathmini viashiria 19 vifuatavyo:

### Uhuru wa Kujieleza na Habari

- F1 (a). Upatikanaji wa sheria na masharti
- F3 (a). Mchakato wa utekelezaji wa sheria na masharti
- F9. Usimamizi wa mtandao
- F10. Mtandao kuzimisha
- F11. Sera ya Utambulisho

### Faragha

- P1 (a). Ufikiaji wa sera za faragha
- P3 (a). Ukusanyaji wa taarifa za mtumiaji
- P3 (b). Hitimisho ya habari ya mtumiaji
- P4. Kushiriki maelezo ya mtumiaji
- P5. Madhumuni ya kukusanya, kukisia, na kushiriki maelezo ya mtumiaji
- P6. Uhifadhi wa maelezo ya mtumiaji
- P7. Udhibiti wa watumiaji juu ya habari zao za mtumiaji
- P8. Ufikiaji wa watumiaji kwa habari zao za mtumiaji
- P10 (a). Mchakato wa kujibu madai ya serikali kwa maelezo ya mtumiaji

P10 (b). Mchakato wa kujibu maombi ya kibinafsi ya maelezo ya mtumiaji

P11 (a). Data kuhusu madai ya serikali kwa maelezo ya mtumiaji

P11 (b). Data kuhusu maombi ya kibinafsi ya maelezo ya mtumiaji

P12. Arifa ya mtumiaji kuhusu maombi ya wahusika wengine kwa maelezo ya mtumiaji

P15. Ukiukaji wa data


Mchakato wa utafiti ulitumia hatua 3 za mchakato wa utafiti wa RDR.

Hatua ya 1: Ukusanyaji Data Msingi: Katika hatua hii, watafiti wa msingi walikusanya data na vyanzo vya kampuni walizopangiwa. Kampuni zilipewa alama kulingana na tathmini ya ufichuzi kwa kila kipengele cha kila kiashirio yaani Ufumbuzi kamili, ufumbuzi wa sehemu, usiopatikana, na hautumiki. Hatua hii ilikuwa muhimu kwa kutoa tathmini ya awali ya utendaji wa kampuni kwa kila kiashirio na kipengele. Data hii iliingizwa katika karatasi za uingizaji zilizoboreshwa kwa kila kampuni.

Hatua ya 2: Mapitio ya Pili: Katika hatua hii, kila mmoja wa watafiti alikagua tathmini za kila mmoja chini ya Hatua ya 1. Hatua hii ilikuwa muhimu kwa kutoa uthibitishaji unaohitajika wa data zote zilizo kusanywa.

Hatua ya 3: Mapitio na Upatanisho: Katika hatua hii, watafiti wote walijadili matokeo kutoka kwa Hatua ya 1 na ya 2. Hatua hii ilikuwa muhimu kwa kutatua tofauti zozote na kukubaliana juu ya matokeo. Ripoti ilitolewa yenye matokeo na uchambuzi wote.

# 04



## Mantiki na mapungufu ya utafiti

### Angola

Kwa kuja kwa kampuni ya nne ya simu nchini Angola, utafiti huu ulilenga kutathmini mojawapo ya watoa huduma mashuhuri waliopo na wanaomilikiwa kibinafsi na mtandao wa simu ambao wana furahia usajili wa juu kiasi, Unitel. Tathmini hii inatumika kuangazia baadhi ya vifungu vyao vya sera vilivyomo katika sheria na masharti yanayopatikana kwa umma (vigezo na masharti), kutambua mapungufu na kutoa taarifa ili kutumika kama msingi wa utafiti na tathmini ya siku zijazo ya mazingira ya mawasiliano nchini huku ikiongeza imani ya watumiaji.


### Jamhuri ya Afrika ya Kati

Nchini Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR), waendeshaaji wa simu wana kiwango cha chini cha miundombinu na ushirikiano. Utafiti kuhusu nchi hii unalenga kutathmini sheria na masharti ya kampuni za simu nchini kuhusu viwango na mazoea ya haki za binadamu, ili kuweka kipaumbele na kuhimiza utiifu wa ahadi za haki za binadamu, kutathmini dhamana na kujenga imani ya mtumiaji. Pamoja na kutoa msingi wa utafiti na tathmini ya siku zijazo za mandhari ya telco nchini. Matokeo ya utafiti huu yanawasilisha kiwango cha kujitolea kwa kampuni ya Orange nchini Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR) kwa masuala ya utawala, uhuru wa kujieleza na faragha.

## Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo

Katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, waendeshaji wanya wawili wameelezea nia yao ya kuwekeza katika soko la TEHAMA nchini Kongo(DRC). Soko kwa sasa inamilikiwa na waendeshaji wanne. Madhumuni ya utafiti ni kutathmini kiwango cha dhamira ya kuheshimu haki za binadamu kwa Opereta Orange ili kuangazia masharti yaliyomo katika sera na masharti ya huduma inayopatikana (vigezo na masharti), kutambua mapungufu ya habari, kutoa msingi. kwa ajili ya utafiti na tathmini ya baadaye ya mandhari ya telco nchini. of this research.

# 05



## Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo

Kwa ujumla, utafiti unaozingatia viwango vya RDR unaonyesha kuwa waendeshaji katika nchi hizi tatu wana mianya mikubwa katika sera zao au masharti ya huduma ambayo yanaweza kukuza ukiukaji wa haki za kidijitali.

Vigezo na masharti ya Unitel Angola yanapatikana kwenye tovuti ya kampuni na yanabainisha kwa uwazi aina za maudhui au shughuli zisizo halali ambazo zinaweza kusababisha vikwazo vya akaunti ya mtumiaji au kusimamishwa kwa huduma. Aidha, sera inatoa utatuzi wa migogoro iwapo kesi kama hiyo itatokea.

Unitel Angola inaonyesha kiwango kizuri cha utiifu wa kuheshimu Faragha, Uhuru wa Kujieleza na Kupata Habari kama ilivyo bainishwa katika Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa.

Unitel Angola haifichui ahadi zake za kutoegemea upande wowote au kueleza ikiwa inatanguliza trafiki ya mtandao.

Unitel Angola haifichui kama inatii matakwa ya serikali ya kuzima mtandao. Hakuna taarifa ya kutosha juu ya maombi ya data na serikali au na makampuni binafsi; wala hakuna ufichuzi wa njia za kufichua idadi ya matakwa yaliyopokelewa ili kuzuia ufikiaji wa huduma au idadi ya kesi zilizokusanywa.

Masharti ya usajili wa SIM ya Unitel Angola

yanahatarisha faragha ya watumiaji wanaohitajika kuthibitisha utambulisho wao kwa kutumia kitambulisho chao cha kitaifa kilichotolewa na serikali, au aina nyingine za utambulisho kwa raia wa kigeni ambao wameunganishwa kwenye utambulisho wao wa nje ya mtandao.

Unitel Angola hufichua kwa uwazi maelezo ya mtumiaji ambayo inakusanya ambayo ni muhimu kwa utoaji wa bidhaa au huduma. Hata hivyo, haibainishi jinsi inavyo kusanya kila aina ya taarifa za mtumiaji au ikiwa taarifa hii inashirikiwa na wahusika wengine, serikali au mamlaka za kisheria.

Watumiaji wa Unitel Angola wana uwezo wa kudhibiti ukusanyaji na utumiaji wa data zao na wako huru kuomba kampuni kudhibiti mchakato wa ukusanyaji, kufuta maelezo ya mtumiaji na kuzima utangazaji unaolengwa.

Unitel Angola haifichui hatua za uhifadhi wa taarifa za mtumiaji na mchakato wa kushughulikia ukiukaji wa data.

Orange ya Jamhuri ya Afrika ya Kati(CAR) na Kongo(DRC) ziko nyuma katika suala la uwazi wa habari kuhusu viashirio muhimu vilivyotathminiwa katika utafiti huu, hasa kuhusu ulinzi wa uhuru wa kujieleza na haki ya kupata taarifa za wafanyakazi na watumiaji wake.

Makampuni hayatoi taarifa zinazopatikana kwa urahisi na watumiaji. Mpangilio wa maelezo haya kwenye tovuti tanzu na kwenye tovuti ya Kampuni ya Mzazi hufanya iwe vigumu kufikia hasa katika lugha nyingine isipokuwa Kifaransa na Kiingereza. Taarifa kwenye tovuti tanzu na kwenye tovuti ya kampuni kuu haiwezi kutafsiriwa kwa urahisi na hivyo kufanya iwe vigumu kwa wasio zungumza Kiingereza au wasi zungumza Kifaransa, ambao wana sehemu ya haki ya idadi ya watu nchini, kupata taarifa.

Orange CAR/DRC haina maelezo ya kutosha kuhusu maombi ya data kutoka kwa serikali au makampuni ya kibinafsi; hakuna mchakato uliobainishwa wa maombi ambayo ni hatari ya jinsi inavyo linda faragha na usalama wa watumiaji wake.

# 06



## Tathmini na Matokeo ya Kampuni

### 6.1. Unitel Angola

#### I. Uhuru wa Kujeleza

Viashirio katika kategoria hii hutafuta ushahidi kwamba kampuni inadhihirisha kuwa inaheshimu haki ya uhuru wa kujieleza na kupata habari, kama ilivyo bainishwa katika Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisia, na vyombo vingine vya kimataifa vya haki za binadamu.

#### **F1 (a). Upatikanaji wa vigezo na masharti: Kampuni inapaswa kutoa masharti ya huduma ambayo ni rahisi kupata na rahisi kuelewa.**

Masharti ya huduma kwa Unitel Group na kampuni ya ndani nchini Angola zote zinapatikana kwenye tovuti za kampuni husika na ni rahisi kupata. Unitel Angola ina sera zinazopatikana katika Kireno ambayo ndiyo lugha kuu nchini humo. Tovuti pia inaoana kikamilifu na zana za kutafsiri tovuti hurahisisha mtu kufikia sera katika lugha yake msingi.

#### **F3 (a). Mchakato wa utekelezaji wa sheria na masharti- Kampuni inapaswa kufichua kwa uwazi mazingira ambayo inaweza kuzuia maudhui au akaunti za watumiaji.**

TSheria na masharti ya Unitel Angola hufichua aina za makosa na maudhui ambayo hayaruhusiwi kwenye mitandao yao na kubainisha hali ambazo inaweza kusimamisha au kuzuia akaunti ya mtumiaji na kwa kiasi, mchakato wa kutatua mizozo iwapo kesi kama hiyo itatokea. Maudhui kama vile bahati nasibu, michezo, ukuzaji wa bidhaa na matukio yakitumika kwa uchunguzi wa biashara wa huduma inayotolewa

na Unitel yanaweza kusababisha akaunti ya mtumiaji kusimamishwa. Aidha makosa kama vile matumizi ya huduma zao kutoa huduma haramu, uvunjaji wa majukumu ya kimkataba, kutoa matamko ya uongo kuhusiana na kitambulisho cha mteja, kushindwa kutoa hati ya utambulisho kwa ajili ya kuambatanishwa na hifadhidata na kwa ujumla, hali yoyote ambayo inaweza kuathiri utendakazi sahihi wa mtandao wao, ubora wa huduma au kesi zinazolingilia maslahi na huduma za kampuni. Kampuni haifichui waziwazi maelezo kuhusu michakato inayotumia kutambua au kuripoti maudhui au akaunti zinazokiuka sheria za kampuni au ikiwa mifumo yoyote ya algoriti inahusika. Hata hivyo, sera inataja uchakataji otomatiki wa maelezo ya mtumiaji.

#### **F9. Usimamizi wa mtandao (kampuni za mawasiliano)-**

Kampuni inapaswa kufichua kwa uwazi kwamba haiwekei kipaumbele, kuzuia, au kuchelewesha aina fulani za trafiki, programu, kikoa au maudhui kwa sababu yoyote ile zaidi ya kuhakikisha ubora wa huduma na kutegemewa kwa mtandao.

Kampuni haifichui ahadi yoyote ya sera ya kutotanguliza kipaumbele, kuzuia, au kuchelewesha aina fulani za trafiki, programu, kikoa au maudhui kwa sababu zaidi ya kuhakikisha ubora wa huduma na kutegemewa kwa mtandao.

#### **F9.3. Ikiwa kampuni itashiriki katika mazoea ya kuweka vipaumbele vya mtandao kwa sababu zaidi ya kuhakikisha ubora wa huduma na kutegemewa kwa mtandao, je, inafichua wazi madhumuni yake ya kufanya hivyo?:**

Kampuni haifichui ikiwa inajihusisha na programu za msamaha wa malipo ambazo zinatanguliza trafiki ya mtandao kwa sababu zaidi ya kuhakikisha ubora wa huduma na kutegemewa kwa mtandao.

#### **F10. Kuzima mtandao (kampuni za**

#### **mawasiliano) -**

Kampuni inapaswa kufichua kwa uwazi mazingira ambayo inaweza kuzima au kuzuia ufikiaji wa mtandao au kikoa, huduma au programu mahususi kwenye mtandao.

Kampuni inafichua wazi kwamba inaweza kuzuia ufikiaji wa mtandao kwa mtumiaji (watumiaji) ikiwa mtu anatumia huduma zao kutoa huduma haramu, ukiukaji wa majukumu ya kimkataba, kutoa matamko ya uwongo yanayohusiana na kitambulisho cha mteja, kushindwa kutoa hati ya kitambulisho kwa kiambatisho. kwa hifadhidata na kwa ujumla, hali yoyote ambayo inaweza kuathiri utendakazi mzuri wa mtandao wao, ubora wa huduma au kesi zinazolingilia maslahi ya kampuni. Zaidi ya hayo, maudhui kama vile bahati nasibu, michezo, ukuzaji wa bidhaa na matukio yakitumika kwa uchunguzi wa kibiashara wa huduma inayotolewa na Unitel hayaruhusiwi na yanaweza kusababisha akaunti ya mtumiaji kusimamishwa.

#### **F10.2. Je, kampuni inafichua kwa uwazi kwa nini inaweza kuzuia ufikiaji wa programu au kikoa maalum (kwa mfano, VoIP, ujumbe) katika eneo fulani au kwa kikundi maalum cha watumiaji?**

Kampuni haifichui kwa nini inaweza kuzuia ufikiaji wa programu au kikoa maalum (kwa mfano, VoIP, ujumbe) katika eneo fulani au kwa kikundi mahususi cha watumiaji.

#### **F10.3. Je, kampuni inafichua wazi mchakato wake wa kujibu matakwa ya serikali ya kufunga mtandao au kuzuia ufikiaji wa huduma?**

Kampuni haifichui mchakato wake wa kujibu madai ya serikali ya kufunga mtandao au kuzuia ufikiaji wa huduma.

#### **F10.4. Je, kampuni inafichua wazi dhamira ya kupinga matakwa ya serikali ya kufunga mtandao au**

### **kuzuia ufikiaji wa huduma?**

Kampuni haifichui ahadi yoyote ya kupinga matakwa ya serikali ya kuzima mtandao au kuzuia ufikiaji wa huduma.

### **F10.5. Je, kampuni inafichua wazi kwamba inawaarifu watumiaji moja kwa moja inapozima mtandao au kuzuia ufikiaji wa huduma?**

Kampuni inafichua wazi kuwa inamjulisha mteja mapema inapozima mtandao au ufikiaji wa huduma.

### **F10.6. Je, kampuni inafichua waziwazi idadi ya madai ya kuzima mtandao inayopokea?**

Kampuni haifichui idadi ya madai ya kuzima mtandao inayopokea.

### **F10.7. Je, kampuni inafichua kwa uwazi mamlaka mahususi ya kisheria inayotoa madai hayo?**

Kampuni haifichui mamlaka mahususi ya kisheria ambayo hutoa madai ya kufunga mtandao au kuzuia ufikiaji wa huduma.

### **F10.8. Je, kampuni inafichua kwa uwazi idadi ya madai ya serikali ambayo ilitekeleza?**

Kampuni haifichui idadi ya matakwa ya serikali ambayo ilitii.

### **F11. Seraya utambulisho - Je, kampuni inahitaji watumiaji kuthibitisha utambulisho wao kwa kitambulisho chao kilichotolewa na serikali, au kwa njia nyinginezo za utambulisho ambazo zinaweza kuunganishwa na utambulisho wao wa nje ya mtandao?**

Kampuni inawahitaji watumiaji kuthibitisha utambulisho wao kwa kutumia kitambulisho chao cha kitaifa kilichotolewa na serikali, au aina nyinginezo za utambulisho, kama vile pasipoti za raia wa kigeni, ambazo zimeunganishwa kwenye utambulisho wao wa nje ya mtandao.

Faragha

### **P1 (a). Ufikiaji wa sera za faragha-**

Kampuni inapaswa kutoa sera za faragha ambazo ni rahisi kupata na rahisi kuelewa. Kampuni haitoi vigezo na masharti ambayo ni rahisi kupata na kufikia kwenye tovuti yao, na pia kuwasilishwa kwa njia inayoeleweka kwa urahisi. Sera zinawasilishwa kwa Kireno, ambayo ndiyo lugha ya msingi inayozungumzwa nchini Angola na ukurasa wa tovuti unaafikiana kikamilifu na zana za kutafsiri hivyo basi kufanya sera kufikiwa na watumiaji wasio Wareno.

### **P3 (a). Mkusanyiko wa habari za watumiaji -**

Kampuni inapaswa kufichua kwa uwazi ni taarifa gani za mtumiaji inazokusanya, na jinsi gani.

Kampuni inafichua wazi ni habari gani inakusanya - jina, anwani, nambari ya simu, barua-pepe na data nyingine yoyote ya mteja muhimu kwa utoaji wa bidhaa au huduma. Hakuna maelezo juu ya jinsi inavyo kusanya kila aina tofauti za maelezo ya mtumiaji. Chini ya 'usalama wa data ya kibinafsi' katika sera ya faragha, data inatumika tu kwa madhumuni ambayo inakusanywa.

### **P3 (b). Hitimisho ya habari ya mtumiaji-**

Kampuni inapaswa kufichua kwa uwazi ni maelezo gani ya mtumiaji inazozingatia na jinsi gani.

Kampuni hufichua kwa uwazi aina zote za maelezo ya mtumiaji yanayotokana na taarifa zilizokusanywa za mtumiaji kama vile jina, anwani, nambari ya simu au barua pepe na data nyingine yoyote muhimu. Kwa kuongezea, Unitel inafichua kwa uwazi kwamba inaweka mipaka ya uelekezi wa maelezo ya mtumiaji kwa yale ambayo ni muhimu moja kwa moja na muhimu ili kutimiza madhumuni ya huduma yake. Hata hivyo, kwa kila aina ya maelezo ya mtumiaji Unitel inakisia, haifichui kwa uwazi jinsi inavyokisia maelezo hayo ya mtumiaji.

## **II. Faragha**

#### **P4. Kushiriki maelezo ya mtumiaji-**

Kampuni inapaswa kufichua kwa uwazi maelezo ya mtumiaji ambayo inashiriki na na nani.

Kwa kila aina ya taarifa ya mtumiaji ambayo kampuni inakusanya haifichui kwa uwazi ikiwa, na aina gani ya taarifa ya mtumiaji inashiriki na wahusika wengine, serikali, mamlaka za kisheria.

#### **P5. Madhumuni ya kukusanya, kukisia, na kushiriki maelezo ya mtumiaji-**

Kampuni inapaswa kufichua wazi kwa nini inakusanya, kupotosha na kushiriki maelezo ya mtumiaji.

Kwa kila aina ya maelezo ya mtumiaji ambayo Unitel inakusanya, inafichua kuwa taarifa za mtumiaji zinakusanywa na kwa madhumuni gani.

#### **P6. Uhifadhi wa taarifa za mtumiaji-**

Kampuni inapaswa kufichua kwa uwazi muda gani ina hifadhi maelezo ya mtumiaji.

Kwa kila aina ya taarifa ya mtumiaji inayokusanywa na Unitel, haifichui kwa uwazi muda gani ina hifadhi maelezo hayo ya mtumiaji na hii inatumika pia kwa maelezo ambayo hayajatambuliwa. Kampuni haifichui ikiwa haitatambua maelezo, inafuta maelezo ya mtumiaji inapofuta akaunti yao au muda ambao inafuta maelezo mara tu mtumiaji anapofunga akaunti yake.

#### **P7. Udhhibiti wa watumiaji juu ya habari zao za mtumiaji-**

Kampuni inapaswa kufichua kwa uwazi kwa watumiaji ni chaguo gani wanazo ili kudhibiti ukusanyaji, makisio, uhifadhi na matumizi ya maelezo ya mtumiaji wa kampuni.

Unitel inafichua kwa uwazi chaguo ambazo watumiaji wanapaswa kudhibiti ukusanyaji, makisio na matumizi ya

taarifa zao za kampuni. Kwa kila aina ya maelezo ya mtumiaji ambayo kampuni inakusanya, kampuni hufichua kwa uwazi ikiwa watumiaji wanaweza kudhibiti mkusanyo wa kampuni wa taarifa hii ya mtumiaji, kufuta maelezo haya ya mtumiaji ikiwa kampuni inaweza kujaribu kupotosha maelezo haya ya mtumiaji, chaguo za kudhibiti jinsi taarifa zao za mtumiaji zilivyo. hutumika kwa utangazaji unaolengwa na utangazaji unaolengwa umezimwa kwa chaguo la msingi.

Kampuni hiyo hata hivyo haisemi ikiwa inawapa watumiaji chaguo za kudhibiti jinsi taarifa zao za mtumiaji zinavyotumika kutengeneza mifumo ya algoriti kwa chaguo la msingi, au la.

#### **P8. Ufikiaji wa watumiaji kwa habari zao za mtumiaji-**

Makampuni yanapaswa kuruhusu watumiaji kupata taarifa zao zote za mtumiaji ambazo kampuni inashikilia.

Kampuni haifichui kwa uwazi ikiwa mtumiaji anaweza kupata nakala ya maelezo yake, aina gani ya maelezo anayoweza kupata, ni aina gani ya muundo wa taarifa hiyo, wala hawezi kufikia maelezo yoyote yanayoonekana kwa umma na ya faragha. Hakuna ufumbuzi wazi ikiwa watumiaji wanaweza kufikia orodha ya kategoria za watazamaji wa utangazaji ambazo kampuni imewapa.

#### **P10 (a). Mchakato wa kujibu madai ya serikali kwa taarifa za watumiaji-**

Kampuni inapaswa kufichua kwa uwazi mchakato wake wa kujibu madai ya serikali kwa maelezo ya mtumiaji.

Unitel haifichui kwa uwazi mchakato wake wa kujibu madai ya serikali isiyoyahakama, amri za mahakama au madai kutoka kwa mamlaka za kigeni. Kampuni haijabainisha misingi ya kisheria ambayo inaweza kufuata matakwa ya serikali wala haifanyi uangalizi unaostahili kwa

madai ya serikali kabla ya kuamua jinsi ya kujibu. Kampuni haifichui ahadi yake ya kurudisha nyuma matakwa yasiyofaa au ya nje ya serikali wala haiweki mwongozo kuhusu mchakato wa utekelezaji wa matakwa ya serikali.

**P10 (b). Mchakato wa kujibu maombi ya kibinafsi ya habari ya mtumiaji-** Kampuni inapaswa kufichua wazi mchakato wake wa kujibu maombi ya maelezo ya mtumiaji ambayo huja kupitia michakato ya kibinafsi.

Kampuni haifichui kwa uwazi mchakato wake wa kujibu maombi yaliyotolewa kupitia michakato ya kibinafsi, msingi wa kutii maombi kama hayo wala haijitolei kurudisha nyuma maombi yasiyofaa au nje ya nchi yaliyotolewa kupitia maombi ya kibinafsi. Kampuni haifichui kwa uwazi ikiwa inatekeleza uangalizi unaostahili kuhusu maombi yanayotolewa kupitia michakato ya kibinafsi kabla ya kuamua jinsi ya kujibu wala kampuni haifichui ikiwa inatoa mwongozo wazi au mifano ya utekelezaji wa mchakato wake wa kujibu maombi yaliyotolewa kupitia michakato ya kibinafsi.

**P11 (a). Data kuhusu madai ya serikali kwa taarifa za mtumiaji-** Kampuni inapaswa kuchapisha mara kwa mara data kuhusu madai ya serikali kwa maelezo ya mtumiaji.

Unitel haiorodheshi au kuchapisha data kuhusu madai ya serikali kwa maelezo ya mtumiaji. Data kama vile idadi ya madai ya serikali ambayo inapokea kulingana na nchi, idadi ya akaunti zilizoathiriwa na aina za mahitaji ni muhimu.

**P11 (b). Data kuhusu maombi ya kibinafsi ya maelezo ya mtumiaji-** Kampuni inapaswa kuchapisha mara kwa mara data kuhusu maombi ya maelezo ya mtumiaji ambayo huja kupitia michakato ya faragha.

Unitel haifichui ikiwa inachapisha mara kwa mara data kuhusu maombi ya maelezo ya mtumiaji ambayo huja kupitia michakato ya faragha wala haifichui idadi ya maombi yaliyopokelewa.

**P12. Arifa ya mtumiaji kuhusu maombi ya wahusika wengine kwa habari ya mtumiaji-**

Kampuni inapaswa kuwaarifu watumiaji kwa kiwango kinachowezekana kisheria wakati taarifa zao za mtumiaji zimedaiwa na serikali na wahusika wengine.

Unitel haifichui kwa uwazi ikiwa inawaarifu watumiaji wakati wahusika wengine kama vile vyombo vya serikali (ikiwa ni pamoja na mahakama au vyombo vingine vya mahakama) na mashirika ya kibinafsi yanapotaka maelezo yao ya mtumiaji.

**P15. Ukiukaji wa taarifa -**

Kampuni inapaswa kufichua hadharani habari kuhusu michakato yake ya kujibu ukiukaji wa data.

Unitel haijafichua kwa uwazi iwapo itaarifu mamlaka husika bila kuchelewa kuchelewa pindi uvunjaji wa data unapotokea, mchakato wa kuwaarifu wahusika wa data ambao wanaweza kuathiriwa na uvunjaji wa data na hatua itakazochukua kukabiliana na athari za uvunjaji wa data kwenye mtandao watumiaji wake.

